TOLEO NA. 07

# TOLEO LATAKWIMU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JANUARI - MACHI, 2026

**IMETAYARISHWA NA**

**KITENGO CHA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII**

**MEI 2026**

## 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia katika kuimarisha takwimu za Matukio ya Kijamii. Miongoni mwa takwimu hizo ni takwimu za Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Toleo la robo ya kwanza ya mwaka 2026 (Januari-Machi), linatoa muhtasari wa takwimu za Matukio ya kijamii. Takwimu hizi zinatolewa kwa mlinganisho wa kijiografia (Wilaya) na kijinsia. Takwimu za Matukio ya Kijamii hutoa taarifa za idadi ya matukio ya kijamii yaliyosajiliwa na Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 2.0 Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za Usajili wa Matukio ya Kijamii za ndani ya Zanzibar. Upatatikaji wa taarifa hizi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya kijamii, kupima mafanikio ya Sera za Afya na kutambua changamoto za kijamii. Aidha, takwimu za matukio ya Kijamii husaidia katika kutathimini maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi, pia hutoa mwongozo muhimu kwa watafiti, serikali, na mashirika ya maendeleo katika kufanya tathimini na maamuzi sahihi kwa jamii. Toleo hili linawasilisha takwimu zifuatazo.

### 2.1 Vizazi Vilivyosajiliwa Ndani ya Wakati

Jadweli Na. 1 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 10,751 vilisajiliwa ndani ya wakati katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026, ambapo wanaume walikuwa 5,066 (47.1%) na wanawake 5,685 (52.9%). Kwa mujibu wa miezi, Januari vizazi 4,340 (40.4%) vilisajiliwa ikijumuisha wanaume 2,001 (46.1%) na wanawake 2,339 (53.9%); Februari vizazi 3,429 (31.9%) vilisajiliwa ikijumuisha wanaume 1,635 (47.7%) na wanawake 1,794 (52.3%); huku Machi vizazi 2,982 (27.7%) vilisajiliwa ikijumuisha wanaume 1,430 (48.0%) na wanawake 1,552 (52.0%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai ulipungua kutoka mwezi Januari hadi Machi, huku wanawake wakibaki kuwa wengi kuliko wanaume katika miezi yote ya kipindi husika.

Kwa ngazi ya wilaya, Jadweli Na. 1 linaonesha kuwa Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vizazi hai 2,154 (20.0%), ikifuatiwa na Magharibi B vizazi 1,385 (12.9%),

Kaskazini A vizazi 1,132 (10.5%), Magharibi A vizazi 1,119 (10.4%) na Chakechake vizazi 1,109 (10.3%). Wilaya nyingine zilikuwa Wete vizazi 1,058 (9.8%), Micheweni vizazi 865 (8.0%), Mkoani vizazi 820 (7.6%), Kusini vizazi 549 (5.1%) na Kati vizazi 386 (3.6%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 174 (1.6%). Kwa ujumla, wilaya nyingi zilionesha idadi kubwa ya wanawake kuliko wanaume, hali inayoendana na mwenendo wa jumla wa takwimu za kipindi hicho.

**Jadweli Na. 1: Usajili wa Vizazi Hai Ndani ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari-Machi 2026**

| Wilaya | Januari-2026 | | | Febuari-2026 | | | Machi-2026 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 174 | 207 | **381** | 195 | 194 | **389** | 172 | 190 | **362** | 541 | 591 | **1132** |
| Kaskazini B | 68 | 60 | **128** | 5 | 11 | **16** | 17 | 13 | **30** | 90 | 84 | **174** |
| Kati | 84 | 91 | **175** | 66 | 58 | **124** | 41 | 46 | **87** | 191 | 195 | **386** |
| Kusini | 101 | 99 | **200** | 93 | 107 | **200** | 76 | 73 | **149** | 270 | 279 | **549** |
| Mjini | 349 | 440 | **789** | 315 | 348 | **663** | 341 | 361 | **702** | 1005 | 1149 | **2154** |
| Magharibi A | 251 | 295 | **546** | 129 | 156 | **285** | 158 | 130 | **288** | 538 | 581 | **1119** |
| Magharibi B | 296 | 318 | **614** | 231 | 242 | **473** | 110 | 188 | **298** | 637 | 748 | **1385** |
| Micheweni | 140 | 196 | **336** | 153 | 136 | **289** | 112 | 128 | **240** | 405 | 460 | **865** |
| Wete | 170 | 174 | **344** | 144 | 181 | **325** | 184 | 205 | **389** | 498 | 560 | **1058** |
| Chakechake | 203 | 275 | **478** | 162 | 210 | **372** | 135 | 124 | **259** | 500 | 609 | **1109** |
| Mkoan | 165 | 184 | **349** | 142 | 151 | **293** | 84 | 94 | **178** | 391 | 429 | **820** |
| **Jumla** | **2001** | **2339** | **4,340** | **1635** | **1794** | **3429** | **1430** | **1552** | **2,982** | **5,066** | **5,685** | **10,751** |

### 2.1.1 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati, Oktoba–Disemba, 2025 na Januari–Machi, 2026

Jadweli Na. 2 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya vizazi hai 13,395 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 6,927 sawa na asilimia 51.7 na wanawake walikuwa 6,468 sawa na asilimia 48.3, hali inayoonesha wanaume kuwa wengi kidogo kuliko wanawake katika kipindi hicho. Wilaya ya Magharibi B iliongoza kwa kusajili vizazi hai 2,417 sawa na asilimia 18.0 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Magharibi A vizazi 2,146 (16.0%), Mjini vizazi 1,485 (11.1%), Kaskazini A vizazi 1,295 (9.7%) na Kati vizazi 1,238 (9.2%). Hata hivyo, Wilaya ya

Kaskazini B ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi hai 306 sawa na asilimia 2.3 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho. Wilaya nyingine zilikuwa Mkoani vizazi 1,140 sawa na asilimia 8.5, Wete vizazi 1,066 (8.0%), Micheweni vizazi 969 (7.2%), Chakechake vizazi 775 (5.8%) na Kusini vizazi 558 sawa na asilimia 4.2 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa ndani ya wakati.

Kwa kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vizazi hai 10,751 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 5,066 sawa na asilimia 47.1 na wanawake walikuwa 5,685 sawa na asilimia 52.9, hali inayoonesha wanawake kuwa wengi kuliko wanaume katika kipindi hicho. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vizazi hai 2,154 sawa na asilimia 20.0 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Magharibi B vizazi 1,385 (12.9%), Kaskazini A vizazi 1,132 (10.5%), Magharibi A vizazi 1,119 (10.4%) na Chakechake vizazi 1,109 (10.3%). Hata hivyo, Wilaya ya Kaskazini B ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi hai 174 sawa na asilimia 1.6 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho. Wilaya nyingine zilikuwa Wete vizazi 1,058 sawa na asilimia 9.8, Micheweni vizazi 865 (8.0%), Mkoani vizazi 820 (7.6%), Kusini vizazi 549 (5.1%) na Kati vizazi 386 sawa na asilimia 3.6 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa ndani ya wakati.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa usajili wa vizazi hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati kutoka vizazi 13,395 katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025 hadi vizazi 10,751 katika kipindi cha Januari–Machi 2026, sawa na upungufu wa vizazi 2,644. Upungufu huo unaweza kuhusishwa na tofauti za mwenendo wa matukio ya vizazi, changamoto za uwasilishaji wa taarifa za usajili kwa wakati, pamoja na mwitikio wa wananchi katika kusajili vizazi ndani ya muda unaotakiwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026.

**Jadweli Na. 2: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati, Oktoba – Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 662 | 633 | **1,295** | 541 | 591 | **1,132** |
| Kaskazini B | 147 | 159 | **306** | 90 | 84 | **174** |
| Kati | 653 | 585 | **1,238** | 191 | 195 | **386** |
| Kusini | 311 | 247 | **558** | 270 | 279 | **549** |
| Mjini | 780 | 705 | **1,485** | 1,005 | 1,149 | **2,154** |
| Magharibi A | 1,142 | 1,004 | **2,146** | 538 | 581 | **1,119** |
| Magharibi B | 1,248 | 1,169 | **2,417** | 637 | 748 | **1,385** |
| Micheweni | 514 | 455 | **969** | 405 | 460 | **865** |
| Wete | 507 | 559 | **1,066** | 498 | 560 | **1,058** |
| Chakechake | 396 | 379 | **775** | 500 | 609 | **1,109** |
| Mkoani | 567 | 573 | **1,140** | 391 | 429 | **820** |
| **Jumla** | **6,927** | **6,468** | **13,395** | **5,066** | **5,685** | **10,751** |

### 2.1.2 Mlinganisho wa Vizazi Hai Vilivyosajiliwa Ndani ya Wakati, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 3 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya vizazi hai 15,821 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 8,225 sawa na asilimia 52.0 na wanawake walikuwa 7,596 sawa na asilimia 48.0, hali inayoonesha wanaume kuwa wengi kidogo kuliko wanawake katika kipindi hicho. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vizazi hai 3,338 sawa na asilimia 21.1 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Magharibi B vizazi 2,204 (13.9%), Chakechake vizazi 1,676 (10.6%), Kaskazini A vizazi 1,525 (9.6%) na Micheweni vizazi 1,525 (9.6%), huku Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 380 sawa na asilimia 2.4. Wilaya nyingine zilikuwa Magharibi A vizazi 1,411 (8.9%), Wete vizazi 1,252 (7.9%), Kati vizazi 1,018 (6.4%), Mkoani vizazi 893 (5.6%) na Kusini vizazi 599 sawa na asilimia 3.8 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa ndani ya wakati.

Kwa kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vizazi hai 10,751 vilisajiliwa ndani ya wakati, sawa na upungufu wa vizazi 5,070 ikilinganishwa na mwaka 2025, ambapo wanaume walikuwa 5,066 sawa na asilimia 47.1 na wanawake walikuwa 5,685 sawa na

asilimia 52.9. Wilaya ya Mjini iliendelea kuongoza kwa kusajili vizazi 2,154 sawa na asilimia 20.0 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Magharibi B vizazi 1,385 (12.9%), Kaskazini A vizazi 1,132 (10.5%), Magharibi A vizazi 1,119 (10.4%) na Chakechake vizazi 1,109 (10.3%). Hata hivyo, Wilaya ya Kaskazini B iliendelea kuwa na idadi ndogo zaidi ya usajili wa vizazi hai 174 sawa na asilimia 1.6 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho. Wilaya nyingine zilikuwa Wete vizazi 1,058 (9.8%), Micheweni vizazi 865 (8.0%), Mkoani vizazi 820 (7.6%), Kusini vizazi 549 (5.1%) na Kati vizazi 386 sawa na asilimia 3.6.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa usajili wa vizazi hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati mwaka 2026 ikilinganishwa na mwaka 2025, sawa na upungufu wa asilimia 32.0. Aidha, mwaka 2026 wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume, tofauti na mwaka 2025 ambapo wanaume walikuwa wengi kidogo. Wilaya zote zilionesha kupungua kwa usajili wa vizazi hai mwaka 2026 ikilinganishwa na mwaka 2025, hususan Wilaya za Mjini, Magharibi B, Micheweni na Chakechake ambazo zilikuwa na upungufu mkubwa zaidi wa usajili katika kipindi hicho.

**Jadweli Na. 3: Mlinganisho wa Vizazi Hai Vilivyosajiliwa Ndani ya Wakati, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 789 | 736 | 1,525 | 541 | 591 | **1,132** |
| Kaskazini B | 184 | 196 | 380 | 90 | 84 | **174** |
| Kati | 553 | 465 | 1,018 | 191 | 195 | **386** |
| Kusini | 302 | 297 | 599 | 270 | 279 | **549** |
| Mjini | 1,734 | 1,604 | 3,338 | 1,005 | 1,149 | **2,154** |
| Magharibi A | 727 | 684 | 1,411 | 538 | 581 | **1,119** |
| Magharibi B | 1,143 | 1,061 | 2,204 | 637 | 748 | **1,385** |
| Micheweni | 801 | 724 | 1,525 | 405 | 460 | **865** |
| Wete | 638 | 614 | 1,252 | 498 | 560 | **1,058** |
| Chakechake | 870 | 806 | 1,676 | 500 | 609 | **1,109** |
| Mkoani | 484 | 409 | 893 | 391 | 429 | **820** |
| **Jumla** | **8,225** | **7,596** | **15,821** | **5,066** | **5,685** | **10,751** |

### 2.1.3 Usajili wa Vizazi Hai Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026, jumla ya vizazi hai 2,007 vilisajiliwa nje ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 1,071 (53.4%) na wanawake 936 (46.6%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vizazi hai nje ya wakati katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa miezi, Januari ilisajili vizazi 649 (32.3%) ikijumuisha wanaume 356 (54.9%) na wanawake 293 (45.1%); Februari ilisajili vizazi 717 (35.7%) ikijumuisha wanaume 365 (50.9%) na wanawake 352 (49.1%); huku Machi ikisajili vizazi 641 (31.9%) ambapo wanaume walikuwa 350 (54.6%) na wanawake 291 (45.4%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa mwezi Februari ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya usajili wa vizazi nje ya wakati ikilinganishwa na Januari na Machi, huku tofauti ya kijinsia ikiwa ndogo zaidi mwezi Februari.

Kwa ngazi ya wilaya, Micheweni ilisajili vizazi vingi zaidi nje ya wakati 430 (21.4%), ikifuatiwa na Mkoani 314 (15.6%), Chakechake 258 (12.9%), Kaskazini A 180 (9.0%) na Kaskazini B 179 (8.9%). Wilaya nyingine zilikuwa Kati 167 (8.3%), Wete 164 (8.2%), Magharibi A 140 (7.0%), Mjini 86 (4.3%), Magharibi B 70 (3.5%) na Kusini 19 (0.9%) ambayo ilisajili idadi ndogo zaidi. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vizazi hai nje ya wakati ulikuwa mkubwa zaidi katika baadhi ya wilaya za Pemba, hususan Micheweni, Mkoani na Chakechake, huku wanaume wakichangia sehemu kubwa ya usajili huu ikilinganishwa na wanawake. Jadweli na. 4.

**Jadweli Na. 4: Usajili wa Vizazi Hai Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-2026 | | | Febuari-2026 | | | Machi-2026 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 24 | 30 | **54** | 42 | 27 | **69** | 37 | 20 | **57** | 103 | 77 | **180** |
| Kaskazini B | 28 | 33 | **61** | 38 | 41 | **79** | 12 | 27 | **39** | 78 | 101 | **179** |
| Kati | 27 | 19 | **46** | 26 | 25 | **51** | 38 | 32 | **70** | 91 | 76 | **167** |
| Kusini | 14 | 4 | **18** | 0 | 1 | **1** | 0 | 0 | **0** | 14 | 5 | **19** |
| Mjini | 4 | 4 | **8** | 27 | 19 | **46** | 16 | 16 | **32** | 47 | 39 | **86** |
| Magharibi A | 12 | 7 | **19** | 27 | 25 | **52** | 35 | 34 | **69** | 74 | 66 | **140** |
| Magharibi B | 5 | 8 | **13** | 16 | 27 | **43** | 10 | 4 | **14** | 31 | 39 | **70** |
| Micheweni | 79 | 85 | **164** | 64 | 72 | **136** | 71 | 59 | **130** | 214 | 216 | **430** |
| Wete | 21 | 14 | **35** | 21 | 25 | **46** | 52 | 31 | **83** | 94 | 70 | **164** |
| Chakechake | 61 | 49 | **110** | 45 | 40 | **85** | 32 | 31 | **63** | 138 | 120 | **258** |
| Mkoan | 81 | 40 | **121** | 59 | 50 | **109** | 47 | 37 | **84** | 187 | 127 | **314** |
| **Jumla** | **356** | **293** | **649** | **365** | **352** | **717** | **350** | **291** | **641** | **1,071** | **936** | **2,007** |

### 2.1.4 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Oktoba – Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 5 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya vizazi hai vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 1,971, ambapo wanaume walikuwa 849 sawa na asilimia 43.1 na wanawake walikuwa 1,122 sawa na asilimia 56.9, hali inayoonesha kuwa wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume katika usajili huo. Wilaya ya Micheweni ilisajili vizazi vingi zaidi 308 sawa na asilimia 15.6 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, ikifuatiwa na Chakechake vizazi 300 (15.2%), Wete vizazi 278 (14.1%), Kaskazini A vizazi 234 (11.9%) na Mkoani vizazi 233 (11.8%), huku Wilaya ya Magharibi A ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 35 sawa na asilimia 1.8. Wilaya nyingine zilikuwa Kati vizazi 204 (10.4%), Magharibi B vizazi 129 (6.5%), Kaskazini B vizazi 127 (6.4%), Mjini vizazi 69 (3.5%) na Kusini vizazi 54 sawa na asilimia 2.7 ya usajili wote wa vizazi hai nje ya wakati.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vizazi hai vilivyosajiliwa nje ya wakati viliongezeka kufikia 2,007, sawa na ongezeko la vizazi 36 ikilinganishwa na kipindi cha

Oktoba–Disemba 2025. Katika usajili huo, wanaume walikuwa 1,071 sawa na asilimia 53.4 na wanawake walikuwa 936 sawa na asilimia 46.6, hali inayoonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika kipindi hicho. Wilaya ya Micheweni iliendelea kuongoza kwa kusajili vizazi vingi zaidi 430 sawa na asilimia 21.4 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, ikifuatiwa na Mkoani vizazi 314 (15.6%), Chakechake vizazi 258 (12.9%), Kaskazini A vizazi 180 (9.0%) na Kaskazini B vizazi 179 (8.9%). Hata hivyo, Wilaya ya Kusini ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 19 sawa na asilimia 0.9 ya usajili wote wa vizazi hai nje ya wakati. Wilaya nyingine zilikuwa Kati vizazi 167 (8.3%), Wete vizazi 164 (8.2%), Magharibi A vizazi 140 (7.0%), Mjini vizazi 86 (4.3%) na Magharibi B vizazi 70 sawa na asilimia 3.5.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa usajili wa vizazi hai nje ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Oktoba–Disemba 2025. Aidha, kumekuwepo na mabadiliko ya uwiano wa kijinsia ambapo wanawake walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, wakati wanaume walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Wilaya za Micheweni, Mkoani, Magharibi A na Chakechake zilionesha ongezeko kubwa la usajili wa vizazi hai nje ya wakati katika mwaka 2026, hali inayoweza kuhusishwa na kuimarika kwa juhudi za uhamasishaji na utoaji wa huduma za usajili katika maeneo hayo.

**Jadweli Na. 5: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Oktoba – Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 102 | 132 | **234** | 103 | 77 | **180** |
| Kaskazini B | 66 | 61 | **127** | 78 | 101 | **179** |
| Kati | 87 | 117 | **204** | 91 | 76 | **167** |
| Kusini | 19 | 35 | **54** | 14 | 5 | **19** |
| Mjini | 31 | 38 | **69** | 47 | 39 | **86** |
| Magharibi A | 14 | 21 | **35** | 74 | 66 | **140** |
| Magharibi B | 59 | 70 | **129** | 31 | 39 | **70** |
| Micheweni | 139 | 169 | **308** | 214 | 216 | **430** |
| Wete | 110 | 168 | **278** | 94 | 70 | **164** |
| Chakechake | 118 | 182 | **300** | 138 | 120 | **258** |
| Mkoani | 104 | 129 | **233** | 187 | 127 | **314** |
| **Jumla** | **849** | **1122** | **1,971** | 1,071 | **936** | **2,007** |

### 2.1.4 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 6 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya vizazi hai vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 3,387, ambapo wanaume walikuwa 1,477 sawa na asilimia 43.6 na wanawake walikuwa 1,910 sawa na asilimia 56.4, hali inayoonesha kuwa wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume katika usajili huo. Wilaya ya Mkoani iliongoza kwa kusajili vizazi 708 sawa na asilimia 20.9 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, ikifuatiwa na Micheweni vizazi 611 (18.0%), Kaskazini A vizazi 516 (15.2%) na Chakechake vizazi 436 (12.9%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 24 sawa na asilimia 0.7. Wilaya nyingine zilikuwa Kati vizazi 276 (8.1%), Wete vizazi 235 (6.9%), Mjini vizazi 187 (5.5%), Kaskazini B vizazi 153 (4.5%), Magharibi A vizazi 134 (4.0%) na Magharibi B vizazi 107 sawa na asilimia 3.2 ya usajili wote wa vizazi hai nje ya wakati.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vizazi hai vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 2,007, sawa na upungufu wa vizazi 1,380 sawa na asilimia 40.7 ikilinganishwa na kipindi cha Januari–Machi 2025. Katika usajili huo, wanaume walikuwa 1,071 sawa na asilimia 53.4 na wanawake walikuwa 936 sawa na asilimia 46.6, hali inayoonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika kipindi hicho. Wilaya ya Micheweni iliendelea kuongoza kwa kusajili vizazi 430 sawa na asilimia 21.4 ya vizazi vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, ikifuatiwa na Mkoani vizazi 314 (15.6%), Chakechake vizazi 258 (12.9%), Kaskazini A vizazi 180 (9.0%) na Kaskazini B vizazi 179 (8.9%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 19 sawa na asilimia 0.9 ya usajili wote wa vizazi hai nje ya wakati. Wilaya nyingine zilikuwa Kati vizazi 167 (8.3%), Wete vizazi 164 (8.2%), Magharibi A vizazi 140 (7.0%), Mjini vizazi 86 (4.3%) na Magharibi B vizazi 70 sawa na asilimia 3.5.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa usajili wa vizazi hai nje ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Januari–Machi 2025. Aidha, kumekuwepo na mabadiliko ya uwiano wa kijinsia ambapo wanawake walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2025, wakati wanaume walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Vilevile, Wilaya ya Micheweni iliendelea kuwa na

mchango mkubwa katika usajili wa vizazi hai nje ya wakati, huku Wilaya za Mkoani, Chakechake na Kaskazini A zikiendelea kuwa miongoni mwa wilaya zenye viwango vya juu vya usajili katika vipindi vyote viwili.

**Jadweli Na.6: Mlinganisho wa Vizazi Hai Vilivyosajiliwa Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari-Machi, 2025 na Januari-Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 191 | 325 | **516** | 103 | 77 | **180** |
| Kaskazini B | 63 | 90 | **153** | 78 | 101 | **179** |
| Kati | 115 | 161 | **276** | 91 | 76 | **167** |
| Kusini | 12 | 12 | **24** | 14 | 5 | **19** |
| Mjini | 88 | 99 | **187** | 47 | 39 | **86** |
| Magharibi A | 51 | 83 | **134** | 74 | 66 | **140** |
| Magharibi B | 47 | 60 | **107** | 31 | 39 | **70** |
| Micheweni | 274 | 337 | **611** | 214 | 216 | **430** |
| Wete | 96 | 139 | **235** | 94 | 70 | **164** |
| Chakechake | 204 | 232 | **436** | 138 | 120 | **258** |
| Mkoani | 336 | 372 | **708** | 187 | 127 | **314** |
| **Jumla** | **1,477** | **1,910** | **3,387** | 1,071 | **936** | **2,007** |

## 2.2 Usajili wa Vifo Ndani ya Wakati

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026, jumla ya vifo 564 vilisajiliwa, ambapo wanaume walikuwa 356 sawa na asilimia 63.1 na wanawake walikuwa 208 sawa na asilimia 36.9, hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa miezi, Januari ilisajili vifo 234 sawa na asilimia 41.5 ya vifo vyote, wakiwemo wanaume 147 (62.8%) na wanawake 87 (37.2%). Februari ilisajili vifo 188 sawa na asilimia 33.3, ambapo wanaume walikuwa 113 (60.1%) na wanawake 75 (39.9%). Aidha, mwezi Machi ulisajili vifo 142 sawa na asilimia 25.2, ukiwemo wanaume 96 (67.6%) na wanawake 46 (32.4%). Takwimu hizi zinaonesha mwelekeo wa kupungua kwa idadi ya vifo kadri miezi ilivyoongezeka, huku wanaume wakiendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika miezi yote mitatu.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Mjini ilisajili vifo vingi zaidi 133 sawa na asilimia 23.6 ya vifo vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Kaskazini A vifo 60 (10.6%), Magharibi B vifo 56

(9.9%), Wete vifo 53 (9.4%) na Magharibi A vifo 52 (9.2%). Wilaya nyingine zilikuwa Mkoani vifo 48 (8.5%), Kusini vifo 46 (8.2%), Chakechake vifo 43 (7.6%), Kati vifo 32 (5.7%), Micheweni vifo 28 (5.0%) na Kaskazini B vifo 13 sawa na asilimia 2.3 ambayo ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vifo vilivyosajiliwa.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha tofauti za kijiografia katika usajili wa vifo, huku Wilaya ya Mjini ikiwa na mchango mkubwa zaidi katika jumla ya vifo vilivyosajiliwa. Aidha, wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo katika kipindi chote cha Januari hadi Machi 2025, Jadweli na. 7.

**Jadweli Na. 7: Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-2025 | | | Febuari-2025 | | | Machi-2025 | | | Jan-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 19 | 5 | **24** | 10 | 9 | **19** | 13 | 4 | **17** | 42 | 18 | **60** |
| Kaskazini B | 2 | 1 | **3** | 4 | 1 | **5** | 3 | 2 | **5** | 9 | 4 | **13** |
| Kati | 6 | 3 | **9** | 10 | 4 | **14** | 6 | 3 | **9** | 22 | 10 | **32** |
| Kusini | 11 | 10 | **21** | 9 | 10 | **19** | 2 | 4 | **6** | 22 | 24 | **46** |
| Mjini | 34 | 20 | **54** | 28 | 18 | **46** | 23 | 10 | **33** | 85 | 48 | **133** |
| Magharibi A | 13 | 9 | **22** | 10 | 6 | **16** | 12 | 2 | **14** | 35 | 17 | **52** |
| Magharibi B | 16 | 15 | **31** | 10 | 5 | **15** | 4 | 6 | **10** | 30 | 26 | **56** |
| Micheweni | 10 | 4 | **14** | 4 | 5 | **9** | 5 | | **5** | 19 | 9 | **28** |
| Wete | 16 | 6 | **22** | 8 | 5 | **13** | 12 | 6 | **18** | 36 | 17 | **53** |
| Chakechake | 8 | 7 | **15** | 7 | 9 | **16** | 7 | 5 | **12** | 22 | 21 | **43** |
| Mkoan | 12 | 7 | **19** | 13 | 3 | **16** | 9 | 4 | **13** | 34 | 14 | **48** |
| **Jumla** | **147** | **87** | **234** | **113** | **75** | **188** | **96** | **46** | **142** | **356** | **208** | **564** |

### 2.2.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Oktoba-Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 8 linaonesha kuwa katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya vifo 654 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 437 sawa na asilimia 66.8 na wanawake walikuwa 217 sawa na asilimia 33.2, hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake katika kipindi hicho. Wilaya ya Magharibi B iliongoza kwa kusajili vifo 181 sawa na asilimia 27.7 ya vifo vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Wete vifo 81 (12.4%), Mjini vifo 79 (12.1%) na Kati pamoja

na Magharibi A zenye vifo 51 kila moja sawa na asilimia 7.8. Hata hivyo, Wilaya ya Micheweni ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 28 sawa na asilimia 4.3. Wilaya nyingine zilikuwa Mkoani vifo 47 (7.2%), Kaskazini A vifo 38 (5.8%), Kusini vifo 36 (5.5%), Chakechake vifo 33 (5.0%) na Kaskazini B vifo 29 sawa na asilimia 4.4 ya vifo vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo vilivyosajiliwa ndani ya wakati vilipungua kufikia 564, sawa na upungufu wa vifo 90 sawa na asilimia 13.8 ikilinganishwa na kipindi cha Oktoba–Disemba 2025. Katika kipindi hicho, wanaume walikuwa 356 sawa na asilimia 63.1 na wanawake walikuwa 208 sawa na asilimia 36.9, hali inayoonesha kuwa wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vifo vingi zaidi 133 sawa na asilimia 23.6 ya vifo vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Kaskazini A vifo 60 (10.6%), Magharibi B vifo 56 (9.9%), Wete vifo 53 (9.4%) na Magharibi A vifo 52 (9.2%). Hata hivyo, Wilaya ya Kaskazini B ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 13 sawa na asilimia 2.3 ya vifo vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho. Wilaya nyingine zilikuwa Mkoani vifo 48 (8.5%), Kusini vifo 46 (8.2%), Chakechake vifo 43 (7.6%), Kati vifo 32 (5.7%) na Micheweni vifo 28 sawa na asilimia 5.0.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa usajili wa vifo ndani ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Oktoba–Disemba 2025. Aidha, wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika vipindi vyote viwili vya usajili wa vifo. Wilaya ya Mjini iliendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa vifo vilivyosajiliwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026, huku Wilaya ya Magharibi B ikiwa na mchango mkubwa zaidi katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025.

**Jadweli Na. 8: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Oktoba-Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 30 | 8 | 38 | 42 | 18 | **60** |
| Kaskazini B | 20 | 9 | 29 | 9 | 4 | **13** |
| Kati | 24 | 27 | 51 | 22 | 10 | **32** |
| Kusini | 15 | 21 | 36 | 22 | 24 | **46** |
| Mjini | 55 | 24 | 79 | 85 | 48 | **133** |
| Magharibi A | 30 | 21 | 51 | 35 | 17 | **52** |
| Magharibi B | 128 | 53 | 181 | 30 | 26 | **56** |
| Micheweni | 24 | 4 | 28 | 19 | 9 | **28** |
| Wete | 53 | 28 | 81 | 36 | 17 | **53** |
| Chakechake | 23 | 10 | 33 | 22 | 21 | **43** |
| Mkoani | 35 | 12 | 47 | 34 | 14 | **48** |
| **Jumla** | **437** | **217** | **654** | **356** | **208** | **564** |

### 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 9 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya vifo 1,331 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 760 (57.1%) na wanawake 571 (42.9%), hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vifo 652 (49.0%), ikifuatiwa na Magharibi B 180 (13.5%), Wete 111 (8.3%) na Magharibi A 94 (7.1%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 17 (1.3%). Wilaya nyingine zilikuwa Kaskazini A 42 (3.2%), Kati 37 (2.8%), Kusini 42 (3.2%), Micheweni 36 (2.7%), Chakechake 61 (4.6%) na Mkoani 59 (4.4%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa karibu nusu ya vifo vyote vilivyosajiliwa vilitokea Wilaya ya Mjini, ikionyesha mkusanyiko mkubwa wa matukio ya vifo katika eneo hilo.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo vilivyosajiliwa ndani ya wakati ilikuwa 564, sawa na upungufu wa vifo 767 (57.6%) ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Katika kipindi hicho, wanaume walikuwa 356 (63.1%) na wanawake 208 (36.9%), hali inayoonesha kuwa wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko

wanawake katika usajili wa vifo. Wilaya ya Mjini iliendelea kuongoza kwa kusajili vifo 133 (23.6%), ikifuatiwa na Kaskazini A 60 (10.6%), Magharibi B 56 (9.9%), Wete 53 (9.4%) na Magharibi A 52 (9.2%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 13 (2.3%). Wilaya nyingine zilikuwa Kati 32 (5.7%), Kusini 46 (8.2%), Micheweni 28 (5.0%), Chakechake 43 (7.6%) na Mkoani 48 (8.5%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa usajili wa vifo ndani ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Aidha, wanaume waliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa katika vipindi vyote viwili. Wilaya ya Mjini imeendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa vifo katika miaka yote miwili, jambo linaloashiria mkusanyiko mkubwa wa matukio ya vifo katika wilaya hiyo ikilinganishwa na wilaya nyingine.

**Jadweli Na. 9: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 29 | 13 | 42 | 42 | 18 | **60** |
| Kaskazini B | 9 | 8 | 17 | 9 | 4 | **13** |
| Kati | 23 | 14 | 37 | 22 | 10 | **32** |
| Kusini | 21 | 21 | 42 | 22 | 24 | **46** |
| Mjini | 373 | 279 | 652 | 85 | 48 | **133** |
| Magharibi A | 48 | 46 | 94 | 35 | 17 | **52** |
| Magharibi B | 97 | 83 | 180 | 30 | 26 | **56** |
| Micheweni | 25 | 11 | 36 | 19 | 9 | **28** |
| Wete | 63 | 48 | 111 | 36 | 17 | **53** |
| Chakechake | 37 | 24 | 61 | 22 | 21 | **43** |
| Mkoani | 35 | 24 | 59 | 34 | 14 | **48** |
| **Jumla** | **760** | **571** | **1,331** | **356** | **208** | **564** |

### 2.1.3 Usajili wa Vifo Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026, jumla ya vifo 91 vilisajiliwa nje ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 61 (67.0%) na wanawake 30 (33.0%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo

nje ya wakati katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa miezi, Januari ilisajili vifo 22 (24.2%) ikijumuisha wanaume 14 (63.6%) na wanawake 8 (36.4%); Februari ilisajili vifo 32 (35.2%) ikijumuisha wanaume 23 (71.9%) na wanawake 9 (28.1%); huku Machi ikisajili vifo 37 (40.7%) ambapo wanaume walikuwa 24 (64.9%) na wanawake 13 (35.1%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa mwezi Machi ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya usajili wa vifo nje ya wakati ikilinganishwa na Januari na Februari.

Kwa ngazi ya wilaya, Chakechake ilisajili vifo vingi zaidi nje ya wakati 18 (19.8%), ikifuatiwa na Magharibi B 16 (17.6%), Magharibi A 14 (15.4%), Wete 9 (9.9%) na Mjini 9 (9.9%). Wilaya nyingine zilikuwa Kaskazini A 7 (7.7%), Kati 6 (6.6%), Micheweni 6 (6.6%), Kaskazini B 3 (3.3%), Mkoani 2 (2.2%) na Kusini 1 (1.1%) ambayo ilisajili idadi ndogo zaidi ya vifo nje ya wakati.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo nje ya wakati ulikuwa mkubwa zaidi katika Wilaya za Chakechake, Magharibi B na Magharibi A. Aidha, wanaume walichangia sehemu kubwa ya usajili wa vifo nje ya wakati ikilinganishwa na wanawake katika kipindi chote cha Januari hadi Machi 2026. Jadweli na. 10.

**Jadweli Na. 10: Usajili wa Vifo Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-2026 | | | Febuari-2026 | | | Machi-2026 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 1 | 2 | **3** | 0 | 0 | **0** | 4 | 0 | **4** | 5 | 2 | **7** |
| Kaskazini B | 0 | 1 | **1** | 1 | 1 | **2** | 0 | 0 | **0** | 1 | 2 | **3** |
| Kati | 1 | 1 | **2** | 1 | 1 | **2** | 1 | 1 | **2** | 3 | 3 | **6** |
| Kusini | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 1 | **1** | 0 | 1 | **1** |
| Mjini | 2 | 0 | **2** | 1 | 0 | **1** | 3 | 3 | **6** | 6 | 3 | **9** |
| Magharibi A | 3 | 1 | **4** | 6 | 2 | **8** | 2 | 0 | **2** | 11 | 3 | **14** |
| Magharibi B | 2 | 2 | **4** | 3 | 1 | **4** | 3 | 5 | **8** | 8 | 8 | **16** |
| Micheweni | 0 | 0 | **0** | 2 | 0 | **2** | 4 | 0 | **4** | 6 | 0 | **6** |
| Wete | 1 | 1 | **2** | 2 | 0 | **2** | 5 | 0 | **5** | 8 | 1 | **9** |
| Chakechake | 3 | 0 | **3** | 7 | 4 | **11** | 2 | 2 | **4** | 12 | 6 | **18** |
| Mkoan | 1 | 0 | **1** | 0 | 0 | **0** | 0 | 1 | **1** | 1 | 1 | **2** |
| **Jumla** | **14** | **8** | **22** | **23** | **9** | **32** | **24** | **13** | **37** | **61** | **30** | **91** |

### 2.1.4 Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Oktoba – Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 11 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya vifo vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 69, ambapo wanaume walikuwa 50 (72.5%) na wanawake 19 (27.5%), hali inayoonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili huo. Wilaya ya Chakechake ilisajili vifo vingi zaidi 17 (24.6%), ikifuatiwa na Mjini na Magharibi B zilizokuwa na vifo 10 kila moja (14.5%), pamoja na Micheweni yenye vifo 9 (13.0%), huku Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B na Kusini zikiwa na idadi ndogo zaidi ya kifo 1 kila moja (1.4%). Wilaya nyingine zilikuwa Kati 5 (7.2%), Magharibi A 5 (7.2%), Wete 7 (10.1%) na Mkoani 3 (4.3%).

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo vilivyosajiliwa nje ya wakati viliongezeka kufikia 91, sawa na ongezeko la vifo 22 (31.9%) ikilinganishwa na kipindi cha Oktoba–Disemba 2025. Katika usajili huo, wanaume walikuwa 30 (33.0%) na wanawake 61 (67.0%), hali inayoonesha kuwa wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume katika kipindi hiki. Wilaya ya Chakechake iliendelea kuongoza kwa kusajili vifo 18 (19.8%), ikifuatiwa na Magharibi A 16 (17.6%), Mjini 14 (15.4%), pamoja na Magharibi B na Wete zilizokuwa na vifo 9 kila moja (9.9%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya kifo 1 (1.1%). Wilaya nyingine zilikuwa Kaskazini A 7 (7.7%), Kaskazini B 3 (3.3%), Kati 6 (6.6%), Micheweni 6 (6.6%) na Mkoani 2 (2.2%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa usajili wa vifo nje ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Oktoba–Disemba 2025. Aidha, kumekuwepo na mabadiliko ya uwiano wa kijinsia ambapo wanaume walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, wakati wanawake walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Wilaya ya Chakechake imeendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa usajili wa vifo nje ya wakati katika vipindi vyote viwili.

**Jadweli Na. 11: Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Oktoba – Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 0 | 1 | **1** | 2 | 5 | **7** |
| Kaskazini B | 0 | 1 | **1** | 2 | 1 | **3** |
| Kati | 5 | 0 | **5** | 3 | 3 | **6** |
| Kusini | 1 | 0 | **1** | 1 | 0 | **1** |
| Mjini | 7 | 3 | **10** | 3 | 11 | **14** |
| Magharibi A | 3 | 2 | **5** | 8 | 8 | **16** |
| Magharibi B | 7 | 3 | **10** | 3 | 6 | **9** |
| Micheweni | 8 | 1 | **9** | 0 | 6 | **6** |
| Wete | 5 | 2 | **7** | 1 | 8 | **9** |
| Chakechake | 11 | 6 | **17** | 6 | 12 | **18** |
| Mkoani | 3 | 0 | **3** | 1 | 1 | **2** |
| **Jumla** | **50** | **19** | **69** | **30** | **61** | **91** |

### 2.1.4 Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Januari – Machi, 2025 na Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 12 linaonesha kuwa, katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya vifo vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 92, ambapo wanaume walikuwa 63 (68.5%) na wanawake 29 (31.5%), hali inayoonesha kuwa wanaume walikuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili huo. Wilaya ya Magharibi B iliongoza kwa kusajili vifo 22 (23.9%), ikifuatiwa na Wete 13 (14.1%), pamoja na Mjini na Micheweni zilizokuwa na vifo 12 kila moja (13.0%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya kifo 1 (1.1%). Wilaya nyingine zilikuwa Kaskazini A 6 (6.5%), Kaskazini B 4 (4.3%), Kati 2 (2.2%), Magharibi A 4 (4.3%), Chakechake 9 (9.8%) na Mkoani 7 (7.6%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa karibu robo ya vifo vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati katika kipindi hicho vilitokea Wilaya ya Magharibi B.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo vilivyosajiliwa nje ya wakati vilikuwa 91, sawa na upungufu wa kifo 1 (1.1%) ikilinganishwa na kipindi cha Januari–Machi 2025. Katika usajili huo, wanaume walikuwa 30 (33.0%) na wanawake 61 (67.0%), hali inayoonesha kuwa wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume katika kipindi hiki.

Wilaya ya Chakechake iliongoza kwa kusajili vifo 18 (19.8%), ikifuatiwa na Magharibi A 16 (17.6%), Mjini 14 (15.4%), pamoja na Magharibi B na Wete zilizokuwa na vifo 9 kila moja (9.9%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya kifo 1 (1.1%). Wilaya nyingine zilikuwa Kaskazini A 7 (7.7%), Kaskazini B 3 (3.3%), Kati 6 (6.6%), Micheweni 6 (6.6%) na Mkoani 2 (2.2%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo nje ya wakati umebakia karibu sawa katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Januari–Machi 2025, huku kukiwa na upungufu mdogo sana wa usajili. Aidha, kumekuwepo na mabadiliko ya uwiano wa kijinsia ambapo wanaume walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2025, wakati wanawake walikuwa wengi zaidi katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Vilevile, Wilaya ya Magharibi B iliyokuwa na mchango mkubwa zaidi mwaka 2025 ilipungua mwaka 2026, huku Wilaya ya Chakechake na Magharibi A zikionesha ongezeko la mchango katika usajili wa vifo nje ya wakati mwaka 2026.

**Jadweli Na. 12: Mlinganisho wa Vifo Vilivyosajiliwa Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Julai-Sept 2025 na Oktoba – Disemba, 2025**

| Wilaya | Januari-Machi, 2025 | | | Januari-Machi, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 4 | 2 | **6** | 2 | 5 | **7** |
| Kaskazini B | 2 | 2 | **4** | 2 | 1 | **3** |
| Kati | 2 | 0 | **2** | 3 | 3 | **6** |
| Kusini | 1 | 0 | **1** | 1 | 0 | **1** |
| Mjini | 7 | 5 | **12** | 3 | 11 | **14** |
| Magharibi A | 4 | 0 | **4** | 8 | 8 | **16** |
| Magharibi B | 12 | 10 | **22** | 3 | 6 | **9** |
| Micheweni | 10 | 2 | **12** | 0 | 6 | **6** |
| Wete | 9 | 4 | **13** | 1 | 8 | **9** |
| Chakechake | 6 | 3 | **9** | 6 | 12 | **18** |
| Mkoani | 6 | 1 | **7** | 1 | 1 | **2** |
| **Jumla** | **63** | **29** | **92** | 30 | **61** | **91** |

## 2.3 Usajili wa Ndoa

Jadweli Na. 13 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya

matukio 288 yalirekodiwa, ambapo Januari ilisajili matukio 58 (20.1%), Februari 42 (14.6%) na Machi 44 (15.3%), hali inayoonesha kuwa Januari ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya usajili ikilinganishwa na miezi ya Februari na Machi. Kwa ujumla, mwelekeo unaonesha kushuka kidogo kwa usajili kutoka Januari hadi Februari, kisha kuongezeka kidogo mwezi Machi.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi A iliongoza kwa kusajili matukio 144 (50.0%), ikifuatiwa na Kusini 36 (12.5%), Mjini 44 (15.3%) na Magharibi B 40 (13.9%), huku Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani zikiwa hazijasajili matukio yoyote katika kipindi hicho (0%). Wilaya ya Kati ilisajili 12 (4.2%), Wete 4 (1.4%) na Chakechake 8 (2.8%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa matukio haya umejikita zaidi katika Wilaya ya Magharibi A ambayo imechangia nusu ya jumla ya usajili wote, huku baadhi ya wilaya zikiendelea kutokuwa na usajili kabisa katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Aidha, mwelekeo wa miezi unaonesha kutokuwa na ongezeko kubwa, bali mabadiliko madogo kati ya miezi mitatu ya kipindi husika.

**Jadweli Na. 13: Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-2026 | Febuari-2026 | Machi-2026 | Januari-Machi, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini B | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 2 | 2 | 12 |
| Kusini | 18 | 0 | 0 | 36 |
| Mjini | 10 | 4 | 8 | 44 |
| Magharibi A | 20 | 32 | 20 | 144 |
| Magharibi B | 6 | 2 | 12 | 40 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 4 |
| 46Chakechake | 0 | 2 | 2 | 8 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | **58** | **42** | **44** | **288** |

### 2.3.1 Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa, Oktoba–Disemba, 2025 na Januari–Machi, 2026

Jadweli Na. 14 linaonesha kuwa katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya ndoa 892 zilisajiliwa Zanzibar. Kati ya hizo, Wilaya ya Kaskazini A ilisajili ndoa 14 sawa na asilimia 1.6 ya ndoa zote zilizosajiliwa, Kaskazini B ndoa 94 (10.5%), Kati ndoa 106 (11.9%), Kusini ndoa 222 (24.9%), Mjini ndoa 24 (2.7%), Magharibi A ndoa 285 (32.0%), Magharibi B ndoa 90 (10.1%), Chakechake ndoa 14 (1.6%), Mkoani ndoa 7 (0.8%), Micheweni ndoa 28 (3.1%) na Wete ndoa 8 sawa na asilimia 0.9. Takwimu hizi zinaonesha kuwa Wilaya ya Magharibi A ndiyo iliyokuwa na mchango mkubwa zaidi katika usajili wa ndoa katika kipindi hicho, ikifuatiwa na Wilaya ya Kusini. Kwa upande mwingine, Wilaya za Mkoani, Wete, Chakechake na Kaskazini A zilikuwa na viwango vya chini vya usajili wa ndoa. Hali hii inaweza kuhusishwa na tofauti za idadi ya watu, kiwango cha uhamaji wa wakazi pamoja na mwamko wa wananchi kuhusu umuhimu wa kusajili ndoa zao kisheria.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya ndoa 1,627 zilisajiliwa, ikiwa ni ongezeko la ndoa 735 sawa na asilimia 82.4 ikilinganishwa na kipindi cha Oktoba–Disemba 2025. Wilaya ya Kati iliongoza kwa kusajili ndoa 600 sawa na asilimia 36.9 ya ndoa zote zilizosajiliwa, ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini ndoa 449 (27.6%), Kusini ndoa 176 (10.8%), Magharibi B ndoa 159 (9.8%) na Magharibi A ndoa 96 (5.9%). Aidha, Wilaya ya Kaskazini B ilisajili ndoa 71 (4.4%), Kaskazini A ndoa 48 (2.9%), Wete ndoa 10 (0.6%), Micheweni ndoa 9 (0.6%), Mkoani ndoa 6 (0.4%) na Chakechake ndoa 3 sawa na asilimia 0.2. Ongezeko hili kubwa la usajili wa ndoa linaashiria kuimarika kwa mwitikio wa wananchi katika kusajili ndoa zao pamoja na uwezekano wa kuongezeka kwa shughuli za kijamii na kiutawala zinazohamasisha usajili wa matukio ya kiraia.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa ndoa umeongezeka kwa kiwango kikubwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ukilinganishwa na Oktoba–Disemba 2025. Aidha, kumeshuhudiwa mabadiliko makubwa katika mgawanyo wa usajili wa ndoa kwa wilaya, ambapo Wilaya za Kati na Mjini zimeonesha ongezeko kubwa la usajili katika kipindi cha Januari–Machi 2026, tofauti na kipindi kilichotangulia ambapo Magharibi A na Kusini ziliongoza. Mabadiliko hayo yanaweza kuashiria kuongezeka kwa

uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa usajili wa ndoa, kuimarika kwa huduma za usajili katika maeneo ya mijini pamoja na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayoathiri mwenendo wa ndoa katika wilaya mbalimbali za Zanzibar.

**Jadweli Na. 14: Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa, Oktoba–Disemba, 2025 na Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | Januari- Machi, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 14 | 48 |
| Kaskazini B | 94 | 71 |
| Kati | 106 | 600 |
| Kusini | 222 | 176 |
| Mjini | 24 | 449 |
| Magharibi A | 285 | 96 |
| Magharibi B | 90 | 159 |
| Micheweni | 28 | 9 |
| Wete | 8 | 10 |
| Chakechake | 14 | 3 |
| Mkoani | 7 | 6 |
| Jumla | **892** | **1,627** |

### 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Januari–Machi, 2025 na Januari–Machi, 2026

Jadweli Na. 15 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya matukio 3,994 yalirekodiwa Zanzibar. Wilaya ya Kaskazini A iliongoza kwa matukio 1,006 (25.2%), ikifuatiwa na Kati 762 (19.1%), Mjini 610 (15.3%) na Magharibi B 483 (12.1%). Wilaya zenye matukio machache zaidi zilikuwa Mkoani 15 (0.4%), Micheweni 26 (0.7%) na Wete 42 (1.1%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa usajili wa matukio ulikuwa mkubwa zaidi katika Wilaya za Kaskazini A, Kati na Mjini.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya matukio yaliyosajiliwa yalipungua hadi 1,627, sawa na upungufu wa matukio 2,367 (59.3%) ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Wilaya ya Kati iliongoza kwa matukio 600 (36.9%), ikifuatiwa na Mjini 449 (27.6%), Kusini 176 (10.8%) na Magharibi B 159 (9.8%). Wilaya za Chakechake 3

(0.2%), Mkoani 6 (0.4%) na Micheweni 9 (0.6%) zilikuwa na idadi ndogo zaidi ya matukio yaliyosajiliwa.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa licha ya kupungua kwa idadi ya matukio yaliyosajiliwa mwaka 2026, bado Wilaya za Kati na Mjini zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika usajili wa matukio. Hii inaonesha uwepo wa tofauti za kijiografia na kiutendaji katika usajili wa matukio kati ya wilaya za Zanzibar, jambo ambalo linaweza kuwa muhimu katika kupanga mikakati ya kuboresha huduma za usajili na kuongeza mwamko wa wananchi katika maeneo yenye usajili mdogo.

**Jadweli Na. 15: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Januari–Machi, 2025 na Januari–Machi, 2026**

| Wilaya | Januari -Machi, 2025 | Januari- Machi, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 1006 | 48 |
| Kaskazini B | 294 | 71 |
| Kati | 762 | 600 |
| Kusini | 194 | 176 |
| Mjini | 610 | 449 |
| Magharibi A | 312 | 96 |
| Magharibi B | 483 | 159 |
| Micheweni | 26 | 9 |
| Wete | 42 | 10 |
| Chakechake | 250 | 3 |
| Mkoani | 15 | 6 |
| Jumla | **3,994** | **1,627** |

## 2.4 Usajili wa Talaka

Jadweli Na. 16 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026, jumla ya talaka 144 zilisajiliwa, ambapo Januari ilisajili talaka 58 (40.3%), Februari 42 (29.2%) na Machi 44 (30.6%), hali inayoonesha kuwa Januari ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya usajili wa talaka ikilinganishwa na miezi ya Februari na Machi. Kwa ujumla, mwelekeo unaonesha kushuka kidogo mwezi Februari kisha kuongezeka tena kidogo mwezi Machi.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi A iliongoza kwa kusajili talaka 72 (50.0%), ikifuatiwa na Mjini 22 (15.3%), Magharibi B 20 (13.9%) na Kusini 18 (12.5%), huku Wilaya ya Kati ikisajili talaka 6 (4.2%) na Chakechake 4 (2.8%). Wilaya ya Wete ilisajili talaka 2 (1.4%), wakati Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani hazikusajili talaka yoyote (0%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa talaka katika kipindi cha Januari–Machi 2026 umejikita zaidi katika Wilaya ya Magharibi A ambayo imechangia nusu ya matukio yote, huku wilaya kadhaa zikiwa hazina matukio kabisa. Aidha, hakuna mwelekeo thabiti wa kuongezeka au kupungua kwa talaka kwa miezi, bali mabadiliko madogo kati ya Januari, Februari na Machi.

**Jadweli Na. 16: Usajili wa Talaka kwa Mwezi Januari–Machi, 2026**

| Wilaya | Januari-2026 | Febuari-2026 | Machi-2026 | Januari-Machi, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini B | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 2 | 2 | 6 |
| Kusini | 18 | 0 | 0 | 18 |
| Mjini | 10 | 4 | 8 | 22 |
| Magharibi A | 20 | 32 | 20 | 72 |
| Magharibi B | 6 | 2 | 12 | 20 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 2 |
| 46Chakechake | 0 | 2 | 2 | 4 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | **58** | **42** | **44** | **144** |

### 2.4.1 Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Oktoba – Disemba, 2025 na Januari–Machi, 2026

Jadweli Na. 17 linaonesha kuwa katika kipindi cha Oktoba–Disemba 2025, jumla ya matukio 120 yalirekodiwa Zanzibar. Wilaya ya Magharibi A iliongoza kwa matukio 40 sawa na asilimia 33.3 ya matukio yote yaliyorekodiwa, ikifuatiwa na Wilaya ya Kati

matukio 24 (20.0%), Kusini matukio 23 (19.2%) na Magharibi B matukio 13 sawa na asilimia 10.8. Aidha, Wilaya ya Mjini ilisajili matukio 11 (9.2%), Kaskazini B matukio 4 (3.3%), Kaskazini A matukio 3 (2.5%) na Chakechake matukio 2 sawa na asilimia 1.7. Wilaya za Micheweni, Wete na Mkoani hazikusajili tukio lolote katika kipindi hicho. Takwimu hizi zinaonesha kuwa usajili wa matukio ulikuwa mkubwa zaidi katika Wilaya za Magharibi A, Kati na Kusini.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya matukio yaliyosajiliwa yaliongezeka hadi 144, sawa na ongezeko la matukio 24 (20.0%) ikilinganishwa na kipindi cha Oktoba–Disemba 2025. Wilaya ya Magharibi A iliendelea kuongoza kwa kusajili matukio 72 sawa na asilimia 50.0 ya matukio yote yaliyorekodiwa, ikifuatiwa na Mjini matukio 22 (15.3%), Magharibi B matukio 20 (13.9%) na Kusini matukio 18 sawa na asilimia 12.5. Aidha, Wilaya ya Kati ilisajili matukio 6 (4.2%), Chakechake matukio 4 (2.8%) na Wete matukio 2 sawa na asilimia 1.4, huku Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani hazikusajili matukio yoyote katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha ongezeko la usajili wa matukio katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Oktoba–Disemba 2025. Aidha, Wilaya ya Magharibi A imeendelea kuwa kinara wa usajili wa matukio katika vipindi vyote viwili, huku Wilaya ya Mjini na Magharibi B zikionesha ongezeko la matukio mwaka 2026. Kwa upande mwingine, baadhi ya wilaya kama Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani zilionesha kiwango cha chini au kutokusajili matukio kabisa katika kipindi hicho.

**Jadweli Na. 17: Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Oktoba – Disemba, 2025 na Januari–Machi, 2026**

| Wilaya | Oktoba-Disemba, 2025 | Januari- Machi, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 3 | 0 |
| Kaskazini B | 4 | 0 |
| Kati | 24 | 6 |
| Kusini | 23 | 18 |
| Mjini | 11 | 22 |
| Magharibi A | 40 | 72 |
| Magharibi B | 13 | 20 |
| Micheweni | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 2 |
| Chakechake | 2 | 4 |
| Mkoani | 0 | 0 |
| Jumla | **120** | **144** |

### 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Jinsi na Wilaya, Januari–Machi, 2025 na Januari–Machi, 2026

Jadweli Na. 18 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari–Machi 2025, jumla ya matukio 383 yalirekodiwa Zanzibar. Wilaya za Kati na Mjini ziliongoza kwa kusajili matukio 85 kila moja, sawa na asilimia 22.2 kwa kila wilaya. Wilaya ya Kaskazini A ilifuatia kwa matukio 77 (20.1%), Magharibi B matukio 51 (13.3%), Kusini matukio 28 (7.3%) na Chakechake matukio 25 sawa na asilimia 6.5. Aidha, Wilaya ya Kaskazini B ilisajili matukio 17 (4.4%), Magharibi A matukio 13 (3.4%) na Mkoani matukio 2 sawa na asilimia 0.5, huku Wilaya za Micheweni na Wete hazikusajili tukio lolote katika kipindi hicho. Takwimu hizi zinaonesha kuwa usajili wa matukio ulikuwa mkubwa zaidi katika Wilaya za Kati, Mjini na Kaskazini A.

Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya matukio yaliyosajiliwa yalipungua hadi 144, sawa na upungufu wa matukio 239 (62.4%) ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Wilaya ya Magharibi A iliongoza kwa kusajili matukio 72 sawa na asilimia 50.0 ya matukio yote yaliyorekodiwa, ikifuatiwa na Mjini matukio 22 (15.3%), Magharibi

B matukio 20 (13.9%) na Kusini matukio 18 sawa na asilimia 12.5. Wilaya ya Kati ilisajili matukio 6 (4.2%), Chakechake matukio 4 (2.8%) na Wete matukio 2 sawa na asilimia 1.4, huku Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani hazikusajili matukio yoyote katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa usajili wa matukio katika kipindi cha Januari–Machi 2026 ikilinganishwa na Januari–Machi 2025. Aidha, kumekuwepo na mabadiliko makubwa katika usajili wa matukio kwa wilaya, ambapo Wilaya za Kati, Mjini na Kaskazini A zilizokuwa zikiongoza mwaka 2025 zilipungua mwaka 2026, huku Wilaya ya Magharibi A ikiongoza kwa kiwango kikubwa cha usajili wa matukio. Hali hii inaashiria kuwepo kwa mabadiliko katika mwenendo wa usajili wa matukio kati ya vipindi hivyo viwili.

**Jadweli Na. 18: Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Jinsi na Wilaya, Januari–Machi, 2025 na Januari–Machi, 2026**

| Wilaya | Januari- Machi, 2025 | Januari- Machi, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 77 | 0 |
| Kaskazini B | 17 | 0 |
| Kati | 85 | 6 |
| Kusini | 28 | 18 |
| Mjini | 85 | 22 |
| Magharibi A | 13 | 72 |
| Magharibi B | 51 | 20 |
| Micheweni | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 2 |
| Chakechake | 25 | 4 |
| Mkoani | 2 | 0 |
| Jumla | **383** | **144** |

### 2.4.2 Uhusiano na Mwenendo wa Ndoa na Talaka

Uhusiano kati ya usajili wa ndoa na talaka katika kipindi cha Januari–Machi 2026 unaonesha kuwa kadiri idadi ya ndoa inavyokuwa kubwa katika baadhi ya wilaya, ndivyo pia idadi ya talaka inavyoonekana kuwa juu zaidi. Katika kipindi hicho, jumla ya ndoa

1,627 na talaka 144 zilisajiliwa Zanzibar. Wilaya ya Kati iliongoza kwa usajili wa ndoa 600 na talaka 6, ikifuatiwa na Mjini ndoa 449 na talaka 22, pamoja na Magharibi A ndoa 96 na talaka 72. Wilaya ya Kusini ilisajili ndoa 176 na talaka 18, huku Magharibi B ikisajili ndoa 159 na talaka 20.

Kwa upande mwingine, wilaya zilizokuwa na kiwango kidogo cha usajili wa ndoa kama Micheweni, Mkoani, Wete na Chakechake pia zilionesha idadi ndogo ya talaka. Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani hazikusajili talaka yoyote katika kipindi hicho, licha ya baadhi yao kuwa na usajili wa ndoa. Hali hii inaonesha uwepo wa uhusiano wa karibu kati ya usajili wa ndoa na talaka, ambapo maeneo yenye idadi kubwa ya ndoa huwa pia na uwezekano mkubwa wa kuwa na talaka nyingi zaidi.

Aidha, Wilaya ya Magharibi A imejitokeza kwa kuwa na uwiano mkubwa wa talaka ukilinganishwa na ndoa zilizosajiliwa, jambo linaloweza kuashiria uwepo wa changamoto za kijamii au mwenendo maalum wa ndoa katika eneo hilo. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa mwenendo wa ndoa na talaka una uhusiano wa moja kwa moja, ambapo ongezeko la shughuli za ndoa katika wilaya fulani huenda sambamba na ongezeko la matukio ya talaka katika kipindi husika. Jadweli na. 19.

**Jadweli Na. 19: Uhusiano na Mwenendo wa Ndoa na Talaka kwa Januari–Machi, 2026**

| Wilaya | Ndoa | Talaka |
|---|---:|---:|
| Kaskazini A | 48 | 0 |
| Kaskazini B | 71 | 0 |
| Kati | 600 | 6 |
| Kusini | 176 | 18 |
| Mjini | 449 | 22 |
| Magharibi A | 96 | 72 |
| Magharibi B | 159 | 20 |
| Micheweni | 9 | 0 |
| Wete | 10 | 2 |
| Chakechake | 3 | 4 |
| Mkoani | 6 | 0 |
| Jumla | **1,627** | **144** |

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla, taarifa za matukio ya kijamii zina umuhimu mkubwa katika kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii, kusaidia maamuzi sahihi ya maendeleo, pamoja na kuchochea ustawi wa jamii kwa ujumla. Usajili sahihi wa matukio hayo husaidia serikali na wadau mbalimbali kupata takwimu muhimu zinazotumika katika upangaji, utekelezaji na tathmini ya mipango ya maendeleo ya Taifa. Hivyo, jamii inahimizwa kushiriki kikamilifu katika kusajili matukio ya kijamii ili kuhakikisha uwepo wa takwimu sahihi na za kuaminika.

Ikumbukwe kuwa takwimu zilizowasilishwa katika taarifa hii ni zile tu zilizosajiliwa rasmi kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA). Hata hivyo, bado kuna matukio mengi yanayotokea katika jamii, hususan vifo, ndoa na talaka, ambayo hayasajiliwi rasmi kwa mamlaka husika. Kutokusajili matukio hayo kunasababisha upungufu wa takwimu muhimu zinazohitajika katika kupanga na kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi. Kutokana na hali hiyo, jamii inasisitizwa kuendeleza utamaduni wa kusajili matukio yote ya kijamii kwa wakati ili kusaidia upatikanaji wa takwimu sahihi zitakazowezesha serikali na wadau wa maendeleo kupanga na kutekeleza mipango yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

## Maelezo Muhimu

- Kizazi hai ni tukio la mtoto kuzaliwa akiwa hai, yaani, mtoto ambaye amezaliwa ana pumzi, anafanya harakati, na ana ishara za maisha. Kizazi hai mara nyingi hufuatana na mchakato wa kawaida wa kujifungua, ambapo mtoto huzaliwa kuja ulimwenguni.
- Kifo ni tukio la mwisho la kuishi. Ni tukio ambalo mwili huacha kabisa kufanya kazi kwa binadamu, kifo hutokea wakati moyo unasimama na kusitisha mtiririko wa damu mwilini, na ubongo kusimama kufanya kazi.
- Usajili ndani ya wakati ni usajili wa matukio muhimu kama vile vizazi, vifo, ndoa au talaka ndani ya muda uliowekwa kisheria baada ya tukio kutokea.
- Usajili nje ya wakati ni usajili wa matukio kama vile vizazi, vifo, ndoa au talaka kusajiliwa baada ya muda uliowekwa kisheria kupita.
- Ndoa ni muungano wa kisheria na kijamii kati ya watu wawili unaotambuliwa na

sheria, mila au dini, kwa lengo la kuishi pamoja kama mume na mke na kuunda familia.

- Talaka ni kitendo cha kisheria cha kuvunja au kusitisha ndoa halali, ambapo wanandoa hawatambuliki tena kama mume na mke mbele ya sheria, dini au jamii.
- Sheria Namba 3 ya 2018, inaeleza kuwa Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ina majukumu ya kusajili Matukio ya kijamii na kutoa vyeti maalum, matukio hayo ni Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Wasiokua Wazanzibari Wakaazi.
- Sheria Namba 9 ya mwaka 2007 inaeleza kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia uendeshaji wa kazi za takwimu katika taasisi zote za Serikali na binafsi zinazofanya shughuli zake hapa Zanzibar.

*Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:*

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI,**
S.L.P 2321, 7 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi,
Zanzibar – Tanzania.
Simu  +255 24 2231869
Faksi: +255 24 2231742
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tz
Website: www.ocgs.go.tz

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMI**
Simu: +255 772 400 597
S.L.P: 264
Barua pepe: info@zcsra.go.tz
Flamingo, Migombani Zanzibar Tanzania.